Vijana wa Biblia

na
M.K. Canner

Kimetafsiriwa Katika Kiswahili na

George Opara na Kikundi Chake
S.L.P. 2245, Kitale, Kenya

Kimehaririwa na Geoffrey K. King'ei

MOMENTS WITH THE BOOK
PO Box 322 • Bedford, PA 15522
(814) 623-8737 • www.mwtb.org

Yaliyomo

Ishmaeli: Hatari ya Kucheza Cheza 3
Isaka: Utiifu kwa Kila Jambo 4
Rebeka: Kuamini na Utiifu 5
Yakobo na Esau: Hadithi Kuhusu Maagano Mabaya 7
Dina: Adhabu ya Kupendwa Sana 9
Yusufu: Je, Utendaji Mema Unayo Faida? 11
Samweli: Kutodharau Mianzo Midogo 13
Daudi: Uwezo wa Imani 14
Yonathani: Kuchagua Marafiki 16
Mefiboshethi: Matumaini kwa Wanyonge 18
Absalomu: Je, Tunahitaji Nini Zaidi ya Msamaha? 20
Sulemani na Yoashi: Mafunzo ya Uongozi 22
Hezekia: Ni Nani Mwenye Jukumu? 24
Yosia: Tazamio la Maana 26
Danieli na Marafiki Zake: Vijana wa Maombi 29
Bikira Maria: Je, Ubikira ni Jambo la Maana? 31
Yesu Akiwa na Umri wa Miaka 12: Maendeleo ya Kiroho Yafaayo 33
Timotheo: Mfano kwa Wazee Wake 35

Ishmaeli

Hatari ya Kucheza Cheza

Wewe umeshawahi kumfanyia mzaha ndugu ama dada yako mdogo? Ishmaeli alijaribu na matokeo yakawa hayafurahishi. Ishmaeli alikuwa mtoto wa Ibrahimu wa mke mtumwa, Hagai. Wakati Ishmaeli alipofika umri wa miaka kumi na minne, Sara, mke wa kweli wa Ibrahimu, alimzaa Isaka. Wakati wa kusherehekea sherehe za kuacha kunyonya kwa Isaka, Ishmaeli alimdhihaki ndugu yake mdogo. Sara aliona tabia za Ishmaeli na siku iliyofuata, Ishmaeli na mama yake, Hagai, walifukuzwa kwenda jangwani wakiwa na akiba haba ya chakula na maji. Wote, Ishmaeli na Hagai wangelifia jangwani; lakini Mungu alikuwa ameahidi Ibrahimu kwamba Ishmaeli angelikuwa baba wa taifa kubwa, kwa hivyo Mungu aliwapa maji (Mwanzo 21).

Somo letu ni nini kutokana na hadithi hii ya Ishmaeli? Isaka wakati mwingine amefikiriwa kuwa kama Kristo na Ibrahimu kama Mungu Baba. Ishmaeli anatukumbusha wale ambao wanachekelea, na kufanya mizaha, au wanakataa mahitaji ya Yesu kwao. Wakati Ishmaeli alipomchekelea Isaka, Isaka alikuwa mtoto asiyejiweza, lakini alikuwa ni mrithi wa mali ya baba yake na mamlaka yake. Yesu wakati huu haonyeshi nguvu zake na mamlaka ulimwenguni, lakini atawahukumu watu siku ambayo inakuja na ni wale tu ambao wamemwamini ndio watakao kuwa warithi pamoja naye (Warumi 8:17). Wale wamalizao maisha yao kwa kumchekelea na kumdharau hawatakuwa na makao katika nyumba ya Baba, bali watatupwa jehanamu, ambalo ni “jangwa” baya sana kuliko yote duniani, na hakuna uponyaji katika mateso hayo. Hakuna uokoaji wa ghafla

kama ule Mungu alioufanya kwa Ishmaeli.

Vijana, labda nanyi pia mwapenda kuchekelea? Mmeshawahi kudharau, au kuchukuwa neno la mungu kimzaha ambapo mliona wazazi au Wakristo wakiwasihi kumgeukia Yesu na kumkubali kama Mwokozi wenu? Chukua ule mfano wa Ishmaeli na ukumbuke ya kwamba, ikiwa huwezi kumkubali Kristo kwa wakati huu, utaishi milele umetengwa kutoka mbele za Bwana na bila matumaini ya kuweza kupokelewa mahali pa baraka.

Isaka

Utiifu kwa Kila Jambo

Ungeweza kufanya nini iwapo ungegundua kwamba baba yako anataka kutoa maisha yako kama sadaka kama moja ya sherehe za kidini? Unaweza kufanya nini wazazi wako wangekwambia ufanye jambo ambalo halikufurahishi? Jibu la Isaka kwa maswali hayo yote lingelikuwa, “Ningetii.”

Wakati Isaka alipokuwa “kijana,” baba yake aliambiwa na Mungu amtoe (Isaka) kama sadaka kwa Bwana (Mwanzo 22). Kisa hiki kilikuwa jaribio la imani ya Ibrahimu na pia lilikuwa jaribio la utiifu wa Isaka kwa baba yake.

Ukitazama maelezo juu ya kujiandaa kwao, Ibrahimu hakumwambia mwanawe Isaka chochote wala Isaka hakumuuliza maswali yoyote. Isaka anafuatana na babake kwa vile ni mapenzi ya baba yake. Ni baada tu ya kumaliza safari yao ndipo Isaka anapouliza swali moja: “Yu wapi mwana kondoo wa sadaka?” Anakubali jibu la baba yake Ibrahimu bila kulalamika, ambalo kwa wengine wetu lingeonekana kama jambo lisilo eleweka vyema. Hata Isaka anapogundua kwamba yeye ndiye sadaka, hashindani,

kulalamika wala kujibizana na baba yake.

Je! vijana, mnatii mamlaka ya wazazi wenu? Kwa kweli hakuna kati yetu alyeulizwa kutii hali kama hii ambayo Isaka alikuwamo. Ibrahimu kwa ufupi alikuwa akitimiza amri ya Mungu, na wazazi wetu, ikiwa ni Wakristo, watatupa mwongozo kama wanavyoelewa mapenzi ya Mungu. Ni mapenzi ya Mungu kwa watoto kutii mamlaka ya wazazi wao (Waefeso 6:1; Wakolosai 3:20). Wazazi wetu wanatupenda na wangependa kutuona tukikua kwa furaha kama Wakristo watiifu, na hutuongoza kutuelekeza katika lengo hili.

Utiifu kwa wazazi ni msingi wa jamii dhabiti na pia familia yenye furaha. Wakati watoto wanapojifunza heshima ya mamlaka nyumbani, watakuwa na heshima kwa serikali na mamlaka ya Mungu, ambalo ni jambo la muhimu kwa wote.

Bila utiifu, maafa hutokea. Dhambi zote na taabu duniani hutukumbusha Adamu na Hawa, kutotii amri ya Mungu. Ghasia na misukosuko humu nchini na katika kila nchi hutokana na kukosekana heshima kwa mamlaka ya wazazi, waalimu, serikali, na hasa mamlaka ya Mungu.

Mwishoni mwa hadithi hii, Isaka hakupoteza maishayake bali alipata baraka nyingi miaka iliyofuata. Kutii mamlaka ya wazazi wetu hakutatuletea balaa bali kutakuwa chanzo cha baraka kwetu tangu sasa na hata maishani mwetu.

Rebeka

Kuamini na Utiifu

Ibrahimu alikuwa amemuuliza mtumishi wake arudi kule ambako Ibrahimu alikokaa zamani, ili amtafutie Isaka

mke kwa jamaa zake. Wakati huo mtumishi alikutana na Rebeka, na akamwona alikuwa msichana mdogo mzuri. Alikuwa amelelewa vizuri na alifanya kazi zake za nyumbani na kutoa huduma hata kwa wale ambao hawajui (Mwanzo 24).

Zaidi ya kuwa kama mfano wa tabia nzuri kwa msichana mdogo, pia alikuwa mfano wa imani kuu pale ambapo mapenzi ya Mungu yamejulikana. Rebeka, baba yake, na ndugu yake walijua papo hapo ya kwamba kukutana kwa Rebeka na mtumishi wa Ibrahimu hakukuwa kwa kawaida. Mungu alikuwa amepanga yote. Hawangelikataa moambi ya mtumishi bila kumkaidi Mungu. Lakini, tunaweza kuuliza, hii ilimaanisha nini kwa tabia ya kibinadamu kwa Rebeka? Angeacha jamii yake yenye furaha alipokulia tangu utotoni. Hakukuwa na chochote cha kuonyesha ya kwamba angeliwaona wazazi au ndugu zake tena. Ingawa Isaka alikuwa tajiri sana kwa ushahidi wa kutoa zawadi kubwa kama hizo ambazo alikuwa ametoa, na pia mtumishi hakuonyesha chochote kuhusu tabia za Isaka. Je, angekuwa mume mzuri kwake? Kwa hakika kulikuweko na watu wa hapo karibu ambao wangelikuwa waume wazuri. Vitu hivi vyote ambavyo vingeliwezekana hakuvifikiria. Mapenzi ya Mungu yalikuwa yamejulikana. Ni uzuri gani kwajibu lake rahisi ya kwamba, “Nitaenda” (mstari 58)!

Ilikuwa ni uzuri gani kwa matokeo ya uamzi wa Rebeka! Siyo tu kuwa mume wake alikuwa tajiri, lakini alimpenda. (Mapenzi hayakuwako kila wakati katika ndoa za kulazimishwa za watu wa jamii za mashariki.) Rebeka alibakia sehemu ya moyo na mapenzi ya Isaka kwa maisha yao yote. Hakuoa wanawake wengine au vimada wengine ingawaje Rebeka alikuwa tasa kwa miaka ishirini. Alikuja akawa mama wa vichwa vya mataifa mawili pamoja na taifa lililoahidiwa na Mungu.

Je, hadithi hii inasema nini kwetu? Tafuta mapenzi ya Mungu kwako, omba kila wakati ili ujue mapenzi yake. Soma Neno la Mungu ambalo atajijulisha kwa mapenzi yake kwako kupitia kwa Roho Mtakatifu. Mungu anajua yale ambayo ni mazuri kwetu, yawe ni uchaguzi wa shule, kazi, au kupata mchumba wa kuishi naye. Panaweza kuwa na pingamizi nyingi za watu dhidi ya mapenzi ya Mungu, lakini lazima tufuate mapenzi ya Mungu. Inaweza kuonekana kwamba tumeacha furaha yote nyuma na tunaenda jangwani mahali pasipojulikana; lakini ikiwa tunafanya mapenzi ya Mungu, kwa hakika atatubariki sana mwishowe. Mwokozi Yesu (ambaye Isaka ni mfano wake) sio tu kuwa vitu vyote viliumbwa kwa uwezo wake, sio tu Mwokozi, lakini pia ni rafiki wetu. Anatupenda; anataka tupate yale yaliyo mazuri kwetu. Mtegemee Mungu kwa uongozi wa kila siku, kila wakati, kwa kila jambo, na utapata maisha ya furaha na yenye afya kiroho.

Yakobo na Esau

Hadithi Kuhusu Maagano Mabaya

Umeshawahi kung'ang'ania kile ulifikiria kwa mawazo yako ni cha thamani lakini baadaye ukatambua ya kwamba si kitu cha thamani? Hicho ndicho kilichofanyika kwa Esau.

Yakobo na Esau walikuwa mapacha, lakini hawakufanana kabisa. Walitofautiana kimaumbile na walikuwa wakipendelea mambo tofauti. Esau alikuwa mwindaji ambaye alikuwa anapenda kuzurura milimani akitafuta wanyama. Yakobo naye alipendelea kukaa nyumbani akichunga kondoo. Siku moja Esau alienda kuwinda, na aliporudi nyumbani, alikuwa na njaa sana.

Yakobo naye alikuwa anapika nyama iliyokaushwa. Esau alimuomba Yakobo ampe nyama kidogo ale; Yakobo alikataa kumsaidia bali alikubali kumwuzia kwa kubadilishana na haki ya kuzaliwa (Mwanzo 25:27-31).

Kabla ya kuendelea na hadithi yetu, labda ningeeleza ni nini maana ya haki ya kuzaliwa. Wakati wa zamani, mtoto mkubwa katika familia alirithi sehemu kubwa ya mali ya baba yake, baba alipokufa. Hii ndiyo iliyokuwa haki ya kuzaliwa kwa mtoto wa kwanza wa kiume. Sasa kwa upande wa Esau, haki hiyo haikuwa tu mifugo na pesa za baba yake bali pia ahadi zote ambazo Mungu alikuwa amempa Ibrahimu: kizazi chake chote kingelikuwa taifa kubwa, Mungu angempa ulinzi maalumu, mataifa yote ya dunia yangelibarikiwa kupitia kwake. (Masiya angetoka katika kizazi hicho), na taifa lake lingepewa Kanaani kuwa nchi yao kabisa (Mwanzo 12:1-3,7). Huu kwa kweli ungelikuwa urithi wa ajabu kuu.

Lakini Esau alifikiria ya kwamba njaa ingelimuua, na hapo hakufikiria lolote lililostahili yeye kufia, kwa hivyo alikubali kuuzia Yakobo urithi wake ili apate kushiba (Mwanzo 25:32-34). Mungu alisema Esau "alidhihaki mamlaka yake ya kuzaliwa." Baadaye wakati Esau alifikiria kile ambacho alikitupa kwa kuuza urithi alilia kwa uchungu; lakini hapakuwa na njia ya kuweza kuirudisha bahati yake ambayo alikuwa amebadilisha na kitoweo kidogo (Mwanzo 27:34-38; Waebrania 12:16,17).

Watu wengi katika dunia hii wanauza matumaini yao ya baraka za milele kwa kitu kisicho cha maana kama hicho kitoweo kidogo. Vitu wanavyo vitaka watu kwa kuuza haki zao hutofautiana kutoka mtu hadi mtu. Wengine hutaka raha, wengine pesa, wengine hutaka tu sifa kwa watu. Lakini watakapofikiria maisha ya milele na kuona kile ambacho wamepoteza, watainua "sauti zao na kulia sana,"

na kugundua ya kwamba haya mambo yote waliyoyatamani hayawezi kulingana na thamani waliyoipoteza.

Mungu anataka sisi sote tupate uzima wa milele. “Alimtoa mwanawe wa pekee ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3: 16). Anatoa uzima wa milele kama zawadi lakini uzima huu ni katika mwanawe, ambaye ni Yesu Kristo (Warumi 6:23) . Ikiwa tunataka uzima wa milele, lazima tukubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Msiwache tamaa zenu kwa vitu vyote vya dunia iwe sababu ya kumdharau Mwokozi wetu Yesu Kristo. Kubadilisha moyo wako na kitu kingine, ni bei ambayo si nzuri. “Itamfaidi nini mtu, kupata ulimwengu wote na mwishowe apoteze roho yake?” (Marko 8:36).

Dina

Adhabu ya Kupendwa Sana

Dina alikuwa hapumziki. Alitaka kukutana na wasichana wa rika lake. Kwa hivyo akaamua aende atembee vijijini labda ingeleta tofauti kidogo ya furaha. Kwa hivyo Dina aliondoka kwenda kuwaangalia wasichana nchini, bila kuandamana na mtu yeyote. Baada ya mda usio mrefu alitumbukia katika taabu na kijana mmoja aliyeitwa Shekemu (Mwanzo 34).

Haijulikani sana ikiwa Dina alishirikiana kwa njia yoyote na Shekemu. Baadaye alitaka kufanya jambo la haki kwa Dina, yaani kumuoa na kumpa nafasi ya kuheshimiwa. Lakini alifanya hivyo kwa njia ya kinyume. Angeliongea na Yakobo kwanza na kumpeleka Dina nyumbani kwake. Alikuwa “ametenda uovu … kitu ambacho hakingelitendeka” (mstari 7).

Ni matokeo gani yaliyo mpata Dina katika safari yake?

Kwanza, alijidanganya mwenyewe. Ndugu zake walisema ya kwamba alikuwa ametendewa tabia za umalaya. Hatujawahi kusoma kuhusu kuolewa kwa Dina au kuzaa watoto kwake, kwa vile ubikira ulichukuliwa kuwa kitu cha maana sana wakati huo wa zamani. (Hakika hatajwi tena ingawaje wanawake wengine wametajwa katika koo mbalimbali.) Pili, ndugu zake walitenda dhambi. Waliafikiana na kumdanganya Shekemu na baba yake na kuuwa watu ambao hawakuwa na hatia. Dina kwa njia nyingine alihusika katika mauaji haya pamoja na mtu aliyempenda. Tatu, baba yake pia aliaibika sana. Alihofia maisha yake. Aliokolewa kutokana na hasira ya majirani zake kwa kitendo cha Mungu kama ilivyoandikwa katika mlango unaofuata.

Vijana wengi Wakristo wamekuwa wakitembea wakitafuta amani, kujifurahisha, na kujulikana. Matembezi kama hayo huwa na mwisho kama ule wa Dina. Ingawa sio desturi ya kisasa kwa ndugu kutetea heshima ya dada yao, bado matokeo ya zinaa ni aibu na tahayari nyingi. “Vitu kama hivyo havitakikani kufanyika.” Kijana anapofanya dhambi, jamii yake nzima huaibika kutokana na dhambi yake.

Enyi vijana, kujulikana katika dunia hakuwezi kulingana na adhabu inayotokea. Hata kama adhabu hiyo si kutenda dhambi, bado patakuwa na kukaribia kutenda dhambi. “Urafiki na ulimwengu ni uadui na Mungu; kwa hivyo anayekuwa rafiki wa ulimwengu ni adui wa Mungu” (Yakobo 4:4). Tunataka urafiki na Mungu au na dunia? Hatuwezi kuwa na urafiki wa aina zote mbili pamqj a. Ni lazima tuchague urafiki na Mungu ndipo tupate furaha. Hakuna yoyote atakayekubali kuitwa adui wa Mungu. Tuhakikishe kwamba wakati huu hatufanyi kama maadui wa Mungu.

Yusufu

Je, Utendaji Mema Unayo Faida?

Maskini Yusufu! Kila alipotenda yaliyo mema, mwingine alimfanyia hila. Je! washangaa wakati mwingine kama kutenda mema kuna manufaa? Pengine hadithi hii ya Yusufu itakupa matumaini.

Yakobo alimpenda Yusufu kuliko wanawe wote (Mwanzo 37:3). Bila shaka Yakobo aliona katika Yusufu jambo ambalo lilikosekana kwa wanawe wengine na pia kwake yeye binafsi, kwa kuwa Yusufu hakuwa na uwongo wala ujanja. Alikuwa mtu asiye na undani na mwaninifu. Hakuwaficha lolote babake na ndugu zake. Aliwaeleza ndugu zake ndoto zake, na kwa kuwa hakuwa na chuki wala ujanja hakutazamia kuwa maono yake yangesababisha matokeo maovu kama hayo kutoka kwa ndugu zake.

Yusufu pia alikuwa amejitoa kikamilifu mbele ya babaye. Yakobo alimwuliza Yusufu aende kuwangalia ndugu zake walipokuwa mbali nyikani wakilisha kondoo (Mwanzo 37:13). Kwa wakati huo, Yusufu alifahamu na pia kusikia hali ya chuki ya nduguze na ukatili wao kwa Shekemu. Angelitarajia ukatili mkali kwa vile alienda pekee yake na bila ya ulinzi. Lakini hakulalamika kwa babaye wala kuogopa, lakini alifanya jinsi babaye alivyomwambia. Ndugu zake walimlipa Yusufu kwa hayo kwa kumuuza kama mtumwa kwa wafanyi biashara walioenda kule Misri.

Tunaona jinsi tabia za Yusufu zilivyofautiana na za ndugu zake. Jibu lake kwa mkewe Potifa linaonyesha jinsi tabia ya Yusufu zilipitana na za dadake Dtna. Alienda duniani, chaguo lake mwenyewe, akitafuta uchumba. Yusufu alikwenda Misri kinyume cha matarajio yake (Misri ni aina moja ya ulimwengu). Dina aliishi katika nyumba

ya Shekemu na kunajisiwa. Yusufu alifungwa jela licha ya kupatikana bila kosa kwa kukataa majaribio. Kuhepa kwa Yusufu na kukataa kusikiliza mawaidha ya mkewe Potifa ilikuwa ni kuchukia kutenda dhambi dhidi ya mapenzi ya Mungu. Alikuwa kijana wa kawaida mwenye tamaa za kimwili. Alikuwa katika nchi ngeni, na aliishi maisha ya kipweke. Lakini alichagua kuishi kwa taabu nyingi jelani kuliko kufanya dhambi ambayo ni kinyume cha mapenzi ya Mungu.

Hatuna nguvu ndani yetu ya kuzuia majaribio ya aina yoyote. Bwana wetu Yesu Kristo anajua shida zetu zote. Yeye hututetea na hata anaweza kutusaidia. Na tuchukie dhambi sana hata tuepuke hali ya hatari kabla haijatufikia.

Na tena, Yusufu aliyatenda mema na akaadhibiwa kwa hayo. Yusufu hangeweza kuepuka jela hata kama angezini. Mkewe Potifa alionekana alikuwa mwanamke mwenye ujanja na hata angemsaliti Yusufu kwa bwanake wakati alikuwa amechoka naye. Yusufu bado angeliendelea kupata adhabu lakini bila usaidizi wa kweli. Lakini Yusufu alikuwa na moyo safi kwa kujua Mungu alipendezwa naye.

Hadithi nyingine yote ya Yusufu twaielewa. Mwishowe alianza kuvuna ukweli ambao alikuwa ameupanda. Wakati alifikisha umri wa miaka thelathini alikuwa wa pili katika mfalme wa Misri. Alipewa mwanamke aliyezaa naye watoto wawili. Mwishowe aliungana tena na babake na ndugu zake. Moyo wa haki wa Yusufu usiobadilika ulimletea majaribu mengi; lakini kwa sababu ya moyo huo, Mungu alikuwa pamoja naye na mwishowe akamfanya mshindijuu ya maadui wake.

Mkumbuke Yusufu unapojaribiwa kuficha mabaya, kudanganya, ama kuingia majaribuni. Mkumbuke unapopatwa na adhabu kwa kuyatenda mema. Mungu

hutubariki tu tunapofanya yale yampendezayo. Yusufu alingojea kwa miaka mingi kabla baraka zake hazijaja. Na hangepokea baraka hizo kama angelifanya mambo tofauti. Yesu alisema, “Heri wanaotaabika kwa ukweli, kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao” (Mathayo 5:10).

Samweli

Kutodharau Mianzo Midogo

Kwa kutimiza ahadi aliyokuwa amefanya kwa Mungu kabla Samweli hajazaliwa, Hana alikuwa amemwacha mwanawe Samweli kwa Eli kuhani mkuu, ili amsaidie Eli katika kazi ya hekaluni. Usiku mmoja, Mungu alizungumza na Samweli alipokuwa mchanga, na akampa ujumbe uliomhusu Eli. Ulikuwa ujumbe mfupi lakini wa kuhangaisha. Eli na wanawe wangalihukumiwa na Mungu kwa ajili ya uovu wa wanawe na kujihusisha kwa Eli na uovu huo. Samweli hakutaka kumwambia Eli ujumbe; lakini Samweli alipoulizwa na Eli, alimwambia yote bila kubakisha (1 Samweli 3).

Ninaamini Mungu alikuwa wakati huu akimtuma Samweli na pia kumpa Eli ujumbe; kwa vile Eli alikuwa amesikia ujumbe wa aina hiyo kutoka upande mwingine (1 Samweli 2:27-36). Mungu alitaka kuwa na hakika kwamba Samweli angalikuwa mwaminifu kwa kutoa neno lake bila kusitasita. Samweli baadaye alikuwa hakimu wa Israeli na nabii wa Bwana kwa miaka mingi, lakini kazi yake ilianza alipomtolea Eli ujumbe huu mfupi.

Ni funzo gani tunalolipata kutokana na kisa hiki cha ujana wa Samweli? Ningalisema hivi: usidharau mianzo midogo. Ingalikuwaje kama Samweli angalidharau au kukataa kumpa Eli ujumbe huo kwa uwoga au kama

angalifikiria kuwa ujumbe huo mfupi si wa maana? Je, Mungu angalimtumia jinsi alivyofanya baadaye? Je, angalikuwa kiongozi wa watu na hata mwenye kuwachagua wafalme wawili wa Israeli pamoja na mzazi wa duniani wa Mfalme wa wafalme? Nafikiri, la. Mungu angalimchagua mtu mwingine kama mjumbe wake.

Mungu hawaanzilishii watumishi wake katika njia inayoonekana. Bali huongeza pole pole katika wajibu aliowapa kulingana na imani katika kazi ile ambayo wako nayo. Ikiwa Mungu amekupa kazi ndogo, ifanye vizuri, na atakuongoza katika kazi kubwa, jinsi unavyozidi kuwa tayari kwa kazi hizo kubwa.

"Akaja wa kwanza, akasema, Bwana, fungu lako limeleta faida ya mafungu kumi zaidi. Akamwambia, Vema, mtumwa mwema, kwa vile ulivyokuwa mwaminifu katika neno lililo dogo, uwe na mamlaka juu ya miji kumi" (Luka 19:16,17).

Daudi

Uwezo wa Imani

Ni mambo gani yanayohitaji ili kuweza kuliua jitu ana kwa ana? Nguvu nyingi, ujuzi wa miaka mingi au silaha kali? Ungependa kukutanishwa na jitu bila silaha yoyote ila teo na imani katika Mungu? Daudi alifanya hivyo na akashinda.

Sisi sote tunajua jinsi Daudi alivyopigana na Goliathi na akashinda (1 Samweli 17). Ni funzo zuri sana kwa shule ya jumapili kwa watoto wadogo lakini ni la manufaa pia kwa watu wa umri wowote. Ni hadithi ya kuridhisha sana kwa sababu Goliathi aliyekuwa na maringo pamoja na silaha zake zote za vita alishindwa kama kitu kidogo

na kijana mchungaji shujaa akitumia teo na jiwe. Sisi sote tungependa kuwa kama Daudi na kuweza kushinda kwa urahisi wale watutishao au wanaotuudhi.

Lakini ushindi wa Daudi haukuwa wa bahati wala matokeo ya maringo ya Goliathi, pekee. Mungu alimsaidia Daudi, na alimsaidia Daudi kwa ajili ya imani yake. Imani ya Daudi ilijaribiwa alipokuwa malishoni akichunga kondoo na alikuwa ameshinda jaribio hilo. Daudi alimtazama Mungu kwa usaidizi ili kuwaua wanyama wakali na Mungu akamwezesha kuwaua.

Daudi akamtukuza Mungu kwa ajili ya ushindi huo na akaamini Mungu atamsaidia anapokutapa na maadui wengine. Sauli alimwahidi Daudi silaha za kupigania lakini Daudi alikataa. Silaha zingekuwa pingamizi kwa mtu aliyejivika silaha ya Mungu.

Ni thamani gani ya Imani Mungu huwahesabia viumbe vyake. “Bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu: yeyote ajaye, kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ni Mungu pekee na Mungu huwapa zawadi wamtafutao bila kuchoka” (Waebrania 11:6). Je! tunatumaini baraka za ajabu maishani mwetu na maishani mwa wapendwa wetu? Miujiza mingi katika Agano Jipya na pia katika Agano la Kale ilikuwa matokeo ya imani. Mungu angali anafanya miujiza leo. Kwa mfano, kuzaliwa upya ni muujiza! Ulinzi wa Mungu katika maisha yetu ya kila siku ni muujiza! Kama mwandishi mmoja alivyosema, ndoa inayodumu kwa miaka mingi na ile, inayobakia kuwa ya kweli na furaha wakati wote, ni muujiza. Tunahitaji imani ili kuzipata baraka hizi na kutambua thamani yake.

Je, tunahitaji ushindi juu ya maadui wetu wa kiroho? Katika Waefeso 6 tumepewa orodha ya silaha za Mungu. Kifungu kimoja ni muhimu kwangu: “Juu ya yote, kuchukua ngao ya imani ambayo inaweza kuzima mishale ya mwovu

Shetani" (mstari 16). Bwana alimwambia Petero, "Shetani amekutamani wewe akupepete kama ngano, lakini nimekuombea kuwa imani yako isikupungukie" (Luka 22:31,32). Imani ni silaha yetu muhimu tunapopambana na Shetani katika uovu wake wote. Kama Daudi, na tukatae mawaidha ya wanadamu na silaha za kimwili, na tukiwa na imani na silaha zingine tulizopewa na Mungu, tuwe nazo tukutanapo na yule adui wetu. "Basi mtiini Mungu. Mpigeni Shetani naye atawakimbia" (Yakobo 4:7)

Yonathani

Kuchagua Marafiki

Yonathani anajulikana kwa uhusiano wake wa kirafiki na Daudi; kwa hakika, majina haya Daudi na Yonathani yakitumika pamoja yamekuwa yakifuatana kwa urafiki wa karibu.

Daudi inaonekana alikuwa mdogo wakati alimuua Goliathi kwa sababu hakuwa mmoja wa askari wa Sauli. (Mtu yeyote wa Israel angeliajiriwa kazi ya askari akiwa na umriwa miaka zaidiya ishirini; Hesabu 1:3.) Yonathani alikuwa mkubwa kuliko Daudi, kwa vile alikuwa amemtumikia baba yake Sauli kwu muda mrefu.

Yonathani alianzisha urafiki na Daudi, halingelikuwa jambo la kawaida kwa Daudi mchungaji mdogo, kufanya uhusiano na mtoto mkubwa katika ufalme. Ni tabia gani ambayo Daudi alikuwa nayo iliyomvutia Yonathani na kuufanya moyo wake kuwa karibu sana na moyo wa Daudi? (1 Samweli 18:1). Aliona kijana mdogo mzuri mwenye nguvu na shujaa. Vitu hivi vilimfanya Daudi kupendwa na watu sana; lakini Yonathani aliona zaidi ya hayo ndani ya

Daudi. Aliona kijana mdogo aliyeamini Mungu kabisa na aliyeweka maisha yake katika ya mikono yake. Yonathani pia alikuwa ni mfano huu wa imani hii ambayo alikuwa ameionyesha wakati alipokuwa katika kambi ya Wafilisti (1 Samweli 14). Uhusiano wa kweli na Mungu na kujitolea kukubali mapenzi ya Mungu viliwaunganisha sana Yonathani na Daudi.

Urafiki wa kweli unaweza kuwako tu, kati ya watu ambao wana maoni sawa juu ya maisha na pia hali moja ya imani. Kwa hivyo Mkristo, inaonyesha, ya kwamba, anaweza kuwa na urafiki wa kweli tu na Mkristo mwingine. Ikiwa mtu angependa kutoa kila sehemu ya maisha yake kwa Bwana, basi atatafuta urafiki wa kweli na watu ambao wanafikiria kama yeye: "Kuna uhusiano gani kati ya haki na wasio haki? Tena pana ushirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye asiyeamini?" (2 Wakorintho 6:14,15). Wakristo wengi wamepoteza nguvu za kiroho na uwezo wa kiroho kwa sababu ya uchaguzi mbaya wa marafiki.

Sisemi ya kwamba tukatae kuwa na uhusiano na wale ambao hawajaokoka. Lakini kupoteza wakati mwingi na wale ambao hawajaokoka ni hasara, labda tu mda huo mwingi unaweza kuutumia kuwaleta kwa Yesu; na kujiingiza katika anasa za kidunia, na shughuli na wale ambao hawajaokoka ni hatari kwa Mkristo na wale ambao sio Wakristo. Mambo kama hayo, hubadilisha fikira na mawazo ya Mkristo na pia huondoa mawazo ya asiye Mkristo katika haja ya kuokolewa. Pamoja na hayo, Mkristo akijiingiza na wasio Wakristo katika ulimwengu, itamfanya asiye Mkristo kujiona ni salama, kumbe sivyo. Asiyeokoka akimuona Mkristo anajiingiza katika mambo ya kidunia, atafikiria ya kwamba yeye sio mwenye dhambi sana, na

ataona kwamba mambo hayo ya kidunia si mabaya.

Mkristo halisi hufanya urafiki na ushirika na wengine ambao wana mawazo kama yake ya kikristo, lakini hatawacha ushirika huo uushinde ule urafiki mkubwa na Bwana wetu Yesu Kristo. Yeye ndiye rafiki wa haki. Yeye anafurahishwa na sisi. Yu tayari kila mara kutusikiliza. Anataka sisi tumwambie yeye furaha yetu na huzuni yetu, ushindi wetu na kushindwa kwetu. Tunaweza kumwambia yeye vitu ambavyo hatutaki marafiki wetu wa kidunia wasikie. (Hatuwezi kumficha yeye jambo lolote.)

Yeye anataka tu baraka zetu na ni yeye tu ambaye anayo hekima na mamlaka ya kupanga kila jambo katika maishayetu ili kutupatia baraka. Ni heri sisi sote tukubali uwezo wake kwetu ili tuweze kushiriki katika baraka hizo.

Mefiboshethi

Matumaini kwa Wanyonge

Baada ya kumshinda Goliathi, Daudi alichukua miaka mingi ya maisha yake akijificha kutoka kwa Sauli, aliyetaka kumuua. Sauli na Yonathani waliuawa katika vita na Wafilistini (1 Samweli 31), na Daudi akawa mfalme wa kabila la Yuda (2 Samweli 2:24). Kwa miaka saba iliyofuata, kulikuweko na vita baina ya wana wa Sauli na wafuasi wake pamoja na jeshi la Daudi. Na mwishowe, mtoto wa Sauli Ishboshethi alipouawa, makabila yote ya Israeli yalimfanya Daudi mfalme (2 Samweli 5:1-4).

Baadaye, Daudi aliuliza ikiwa uzao wowote wa Sauli ulikuwa umebakia ili awaonyeshe huruma kwa ajili ya upendo ambao Daudi alikuwa nao kwa Yonathani. Yule tu aliyepatikana alikuwa Mefiboshethi mtoto wa Yonathani (2 Samweli 9:1-3). Mefiboshethi alikuwa amepooza tangu

utotoni alipokuwa na umri wa miaka mitano. Mlezi wake alimwangusha wakati alikuwa anatoroka kutoka nyumbani wakati walisikia habari ya kwamba Yonathani ameuawa. Ingawaje Mefiboshethi alikuwa kiwete, Daudi alimuwekea urithi wote wa Sauli na Yonathani na akamualika ale naye katika meza ya kifalme. Na "Mefiboshethi, akasema mfalme,... atakula kwenye meza moja na mimi, kama mmoja wa wototo wa mfalme" (2 Samweli 9:11).

Daudi anaitwa mfano wa Yesu na kisa hiki cha Mefiboshethi ni kama ule mfano wa Kristo juu ya wenye dhambi. Daudi alikuwa ameteseka sana kutokana na babu ya Mefiboshethi. Wakati mwingine mfalme mpya angeiua jamii yote ya mfalme wa zamani ambaye amependuliwa ili kusiwe na wengine ambao wanaweza kumpokonya ufalme wake. Lakini Daudi alimfanyia Mefiboshethi huruma kwa sababu ya upendo wa baba yake na pia mtoto wake. Mwokozi wetu Yesu Kristo aliteseka mikononi mwa wenye dhambi. Mungu angelituhukumu sisi sote kwa sababu ya uovu wetu, lakini akafanya njia ya wokovu kwetu kupitia kwa kifo cha Yesu Kristo.

Mefiboshethi alikuwa kiwete na hangemtumikia Daudi kwa njia yoyote. Vivyo hivyo, hakuna njia yoyote tunayoweza kujipatia wokovu, kwa sababu hatujiwezi. Sisi ni wenye dhambi. Lazima tukubali, wokovu kama msaada mkubwa kutoka kwa Mungu, kama vile Mefiboshethi alivyokubali huruma ya Daudi na ukarimu wake. Mefiboshethi alikula na Daudi kama mmoja wa watoto wa mfalme. Sisi ambao tumemkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi, tunafanywa kuwa watoto wa Mungu (Yohana 1:12) na tumekaa pamoja na Kristo mbinguni machoni pa Mungu (Waefeso 2:6).

Na kama Mefiboshethi angekuwa na kiburi na akakataa ukarimu wa Daudi. Angebaki masikini na asiyejiweza

katika maisha yake yote. Ikiwa yeyote atakataa kukubali msaada huu wa uzima wa milele kupitia kwa imani ya Yesu Kristo, atakosa kuwa na furaha ya kujua Yesu Kristo katika maisha haya, na ametenganishwa na Mungu milele baada ya maisha haya. Je, kama Mefiboshethi angelikataa kumtambua Daudi kama mfalme, na alikuwa amejaribu kujinyakulia ufalme huo mwenyewe? Daudi angemuua kwa hatia ya uhaini. Kwa hivyo yeyote anayekataa kumkubali Yesu kama Mwokozi na Bwana, anasema, "Sitakubali huyu mtu, Yesu kuwa mfalme wangu. Nataka nijitawale mimi binafsi." Mungu atahukumu mtu kama huyu milele kwa sababu amekataa mwanawe ambaye ndiye mfalme wa wafalme. Huwezi kukubali Bwana wetu Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako na ufurahie baraka ambazo amekuwekea?

Absalomu

Je, Tunahitaji Nini Zaidi ya Msamaha?

Kila mara tunasikia watu wakisema, "Siamini ya kwamba Mungu atatupa au atapeleka watu jehanamu kabisa"; au, "Ninaamini ya kwamba watu wakifanya mabaya, wanaadhibiwa katika maisha haya ya sasa, na kwamba Mungu anasamehe kila mwanadamu baada kufa"; au, "Atapewa nafasi nyingine baada ya kufa." Tunafahamu kulingana na maandiko matakatifu ya kwamba hakuna ukweli katika maelezo haya yote, lakini maisha ya Absalomu yanatuoenyesha kwa nini Mungu hawezi kumsamehe mtu mara moja kwa urahisi.

Absalomu alikuwa kijana mdogo mzuri wa kupendeza, na alikuwa na dada yake mrembo ambaye aliitwa Tamari. Ndugu yake wa kambo ambaye ni Amnoni alimkosea

vibaya Tamari na Absalomu akamchukia kwa kitendo hicho. Wakati Daudi alisikia juu ya dhambi hiyo ya Amnoni, alipata hasira sana lakini hakuna alilolifanya; Absalomu naye akaamua kumuwa Amnoni. Absalomu alikimbilia nchi jirani kwa miaka mitatu. Daudi naye alitaka kumrudisha Absalomu nyumbani ingawaje Absalomu alikuwa ametenda dhambi (2 Samweli 13).

Mwishowe Daudi alimrudisha Absalomu kule Yerusalemu, lakini alikataa kumuona. Absalomu aliona hawezi kuvumilia jambo hilo na baada ya miaka miwili kule Yerusalemu, alimulazimisha Yoabu kwenda kuongea na Daudi. Na hapo Daudi alimuita Absalomu mbele yake na akambusu. Na hapo Absalomu akarudia kiti chake kama mwana wa mfalme.

Katika mlango wa kumi na tano (15), na ishirini (20) katika 2 Samweli, mna maelezo ya kuhuzunisha sana katika Agano la Kale. Absalomu alianzisha mapinduzi dhidi ya Daudi na ilimlazimu Daudi akimbie Yerusalemu, na Absalomu akanyakua ufalme huo. Absalomu aliuawa baadaye, ingawa kulikuweko na umwagikaji wa damu kabla ya mzozo huo kuzimwa kabisa.

Daudi alimsamehe Absalomu ingawa Absalomu hakutubu ama kuonyesha masikitiko yoyote juu ya dhambi zake. Tamaa ya Absalomu kumuona mfalme haikuwa ya upendo kwa Daudi, lakini ni kwa sababu alitaka apate nafasi ambayo angeungwa mkono, au kutafuta waafuasi. Absalomu alikuwa amechukua mamlaka yote ya Daudi wakati alimuua Amnoni.

Wanaondelea kutenda dhambi ni waasi mbele za Mungu (Warumi 8:7,8). Haja zao ni kujifurahisha wao wenyewe lakini si Mungu. Kama ni Wakristo watenda dhambi wanaweza kuongea juu ya kumtumikia Mungu na kumuabudu; lakini wanatarajia kufanya mambo hayo kwa

njia yao wenyewe, lakini si kwa kufuata njia ya Mungu. Mungu anawezaje kumsamehe mwenye dhambi asiyetubu? Absalomu hakuonyesha upendo wowote au shukurani yoyote kwa msamaha wa Daudi kwake. Wale ambao hawajaokoka pia wanaweza kukosa upendo, na shukurani kwa Mungu kama akiwasamehe bila wao kutubu. Uasi wao ungejitokeza kule mbinguni kama Mungu angewaruhusu waingie bila kutubu, kama vile Absalomu aliasi dhidi ya baba yake baada ya kutoka mafichoni kule Yerusalemu.

La, wenye dhambi lazima watubu (na wazaliwe mara ya pili). Na lazima watubu katika maisha haya. Hakutakuweko na nafasi ya kutubu katika jehanamu, kwa sababu Roho Mtakatifu ambaye analeta kutubu katika moyo hatakuwa akifanya kazi kule kuzimu. "Mungu … sasa anaamuru watu wote kila mahali watubu" (Matendo 17:30). Tunahitaji zaidi ya kusamehewa (kuondolewa hukumu ya dhambi); tunahitaji tuwe huru kutokana na nguvu za dhambi, tuondolewe kwa dhambi zote na tupewe maumbile mapya ya upendo na kumtii Mungu. Hapo tu, ndipo tutakuwa tunastahili mbele za Mungu na kuishi naye milele.

Sulemani na Yoashi

Mafunzo ya Uongozi

Sulemani amezungumziwa kuwa mdogo sana wakati alipoanza kutawala (1 Wafalme 3:7; 1 Nyakati 29:1) ingawaje hatujapewa umri wake hasa. Alitambua mahitaji yake na wakati Mungu alimuuliza aombe anachohitaji, Sulemani alichagua hekima na maarifa ndipo aweze kuongoza watu wa Mungu (1 Wafalme 3 na 2 Nyakati 1). Mungu alifurahia uamuzi wa Sulemani na akampa kile ambacho aliomba na pia ambavyo hakuomba. Mungu alizidi kumuongezea

kama vile mali na utukufu.

Yoashi, ambaye alianza uongozi wake akiwa na umri wa miaka saba, pia alikuwa na mahitaji. Alitaka apate mtu ambaye angempa mawaidha ili aongoze vizuri. Wakati mjomba wake Yehoyada alikuwa hai, alimtumikia Mungu. Wakati mjomba wake alikufa, upungufu wa tabia zake ulijitokeza. Alirudia wale watu ambao hawana mawaidha ya busara (2 Nyakati 24:17-19) ambao walimwelekeza kwa miungu wengine. Mungu aliwatuma manabii na mwana wa Yehoyada ambaye aliitwa Zekaria kumwambia mapenzi ya Mungu, lakini aliwapuuza manabii na akamuua Zekaria. Kwa sababu ya uovu wake Mungu aliwatuma wa-Syria kuvamia Yerusalemu na Yoashi mwenyewe aliuwawa na watumishi wake akiwa na miaka 47. Ni furaha gani angelipata kama angelimtazama Mungu kwa mahitaji na mwongozo wa kila aina ambao angelihitaji.

Sulemani na Yoashi walijua hali ya maisha yao jinsi yangelikuwa lakini walihitaji uongozi wa Mungu ndipo waendelee vyema. Tunahitaji uongozi wa Mungu ili tuchague kazi nzuri na pia uongozi wake ili tufanye vyema. Sasa Mungu anafahamu kushindwa kwetu, pia mahitaji yetu, pia vipawa vyetu, na nguvu zetu. Anafahamu ni kazi gani inafaa kila mmoja wetu. Sio tu kwamba kazi tofauti zinahitaji ujuzi tofauti, lakini kazi zingine huleta majaribu mbali mbali na pia huzuia maendeleo ya kiroho. Ikiwa tutamuachia yeye Mungu kutuchagulia, tutapata kazi ambayo inatufaa na iwezayo kutukuza kiroho. Mahali ambapo atatuchagulia hapatutapitia heshima ya kiulimwengu sana, lakini patakuwa mahali ambapo tunaweza kumtumikia vyema zaidi.

Wakristo wengi watatambua ya kwamba, lazima tumtazamie Mungu ili kutuongoza kwa kila ambacho kinaitwa “kazi ya Mungu.” Ni wachache watambuao

kwamba ni lazima kumtazamia Mungu kutuonyesha ama kutuongoza katika "kazi za kidunia." Lakini Mkristo ambaye ameokoka hawezi kuona tofauti kati ya kazi za Mungu na kazi za kidunia katika maisha yake. Lazima amtumikie Mungu hata kama anajenga hema au anahubiri injili. Hapatakikani paweko na mtu ambaye anajiita "Mtumishi wa mda wa Mungu."

Fikira za wale ambao hupata mahitaji yao kutokana na "kazi za duniani" zinapasa kuwa: "Watumishi na wawe watiifu kwa wakubwa wao ambao wanawatawala kimwili kwa kuwaogopa na kutii, kwa unyofu wa mioyo yao kama vile kwa Kristo, sio tu kushiriki na macho, au kufurahisha watu, lakini kama watumishi wa Yesu, na kufanya mapenzi yake, kwa moyo mmoja" (Waefeso 6:5,6). Mungu anaweza kutusaidia kutatua matatizo ambayo tunakutana nayo katika kazi zetu. Ikiwa tutatafuta mapenzi yake kila wakati, siku baada ya siku, kazi zetu zitaendelea vyema.

Imetupasa kumtumikia Mungu kwa kila kazi katika maisha yetu yote. Ikiweko shughuli yoyote ambamo hatumtumikii Mungu, tuwache shughuli hiyo. Lazima kwa kila kazi katika maisha yetu, iwe ni kazi ya kumsifu Mwokozi wetu Yesu Kristo.

Hezekia

Ni Nani Mwenye Jukumu?

Huwezi kujisaidia ikiwa maisha yako hayako vile yanatakiwa kuwa. Wazazi wako, waalimu, na mazingira uliyomo kwa jumla yamekufanya uwe vile ulivyo, kweli? La, maisha ya Hezekia yanasema, "Sio Hivyo."

Kama vile wafalme wengi wa Yuda, Hezekia alikuwa kijana mdogo wakati alianza utawala wake. Utawala

wake ulikuwa na mwelekeo wa kumtegemea Mwokozi; na ilikuwa imejulikana kwa sababu Hezekia alianza utumishi wake kwa Mungu bila kusitasita katika mwezi wa kwanza kwa uongozi wake. Inaelekea ya kwamba Hezekia alikuwa amechukizwa na uovu ambao uliendelea wakati wa utawala wa baba yake Ahazi, na alijaribu kuepuka hayo haraka iwezekanavyo (2 Wafalme 18).

Maisha ya Hezekia ni ushuhuda dhidi ya filosofia ya sasa kuwa vijana wa siku hizi ambao hufanya uovu, hawawezi kulaumiwa kwa makosa yao; ya kwamba ni watu wasio na hatia, wenye wazazi wanafiki, ambao hawajali, kukosa elimu au mazingira mabaya. Ikiwa mtu atakuwa na sababu kama hizo, Hezekia pia angekuwa nazo. Baba yake alikuwa amehusika katika ibada za sanamu. Kila mtu karibu naye alikuwa hivyo hivyo. Baba yake alikuwa hajakomaa wakati Hezekia alipozaliwa na ni Mama yake tu aliyempa mwongozo ufaao. Lakini Hezekia alitambua kwamba Mungu hangelikubali visingizio. Mbele ya Mungu kila mtu ana wajibu juu ya matendo yake binafsi. Hezekia alianza tangu mwanzoni kufanya mapenzi ya Mungu.

Mimi sijaribu kupunguza uwezo wa wazazi kulea watoto ili wampendeze Bwana Yesu, wala sijaribu kukataa ya kwamba wazazi wengi wameshindwa kuchukua jukumu lao kwa njia hii au ile. Lakini hata kama wazazi wetu wamefanya vibaya kwa kila jambo, Mungu anatuhitaji kumtii, na hata kumtii wakati wa ujana wetu.

Ikiwa tuko radhi kwa mapenzi ya Mungu kwetu, ili Mungu atachukua kudhoofika kule kwa wazazi wetu kuleta baraka kwetu. Kwa kuangalia udhaifu wao tutaweza kuwa wazazi wazuri. Tunaweza kuwahurumia wengine ambao wamekuwa na hali mbaya kama yetu.

Mungu ana mahali ambapo ametuandalia kila mmoja wetu katika Kanisa lake na kila ujuzi ambao tuko nao ni

Mungu ambaye ametupa ili utufae katika mahali ambapo ametuandalia. Kwa kuwalaumu wazazi wetu na kushindwa kutekeleza mahitaji ya Mungu kwetu, tunakosa baraka kubwa ambazo Mungu ametupangia.

Yosia

Tazamio la Maana

Kuna mafunzo mengi ambayo vijana wanaweza kujifunza kutokana na maisha ya Yosia. Ingawaje alikuwa Mfalme wa Yuda kwa miaka 31, alikuwa bado kijana mdogo kwa umri wakati alipokufa akiwa na miaka 39.

Hatujaambiwa chochote kuhusu uongozi wake katika miaka minane ya mwanzo. Ilikuwa miaka ya maana kwa Yosia (na pia nchi ya Israel) kwa sababu baada ya mda huo, “Yosia alianza kumtazama na kumtafuta Bwana, ambaye ni Mungu wa baba yake Daudi” (2 Nyakati 34:3). Ni kitu gani kilimlazimisha amgeukie Mungu wa baba zake wakati nchi nzima ilikuwa imegeukia ibada ya sanamu? Haikuwa ni kulisoma Neno la Mungu, kwani inaonekana kuwa Yosia alipata chuo cha agano kutoka hekaluni baada ya miaka kumi na minane ya uongozi wake. Labda ilikuwa ni juhudi za mama yake au mawaidha kutoka watu ambao walikuwa wamemtambua Bwana. Yosia alikuwa na umri wa miaka 16 wakati alimgeukia Mungu. Yosia hakukawia kufanya uamzi huu wa maana katika maisha yake. Ingawaje maisha yake yalikuwa mafupi sana, alikuwa na miaka mingi ya kumtumikia Mungu kwa sababu alimtambua wakati alikuwa angali kijana. Hakuna katika sisi ajuaye mda atakaoishi hapa duniani. Tusipoteze mda wowote au kuchelewa kupokea uzima wa milele kwa kuchelewa kumkubali Yesu mpaka wakati ambapo tumekuwa wazee.

Miaka minne baada ya Yosia kuanza kumtafuta Bwana alianza kazi yake ya kuondoa nchi ya Yuda katika ibada za sanamu. Hakuharakisha kuanza kazi kabla ya kuheshimu na kumpenda Mungu. Wakristo wote imewapasa waige mtindo wa kumtegemea Bwana ili wajifunze mapenzi ya Mungu kwao, na wawe na msimamo thabiti katika Neno lake kabla ya kuchaguwa kazi yoyote ya Mungu. Urefu wa mda huu ni tofauti kwa kila mtu, kufuatana na umri wake na kiasi cha kukomaa kwake wakati wa kuokolewa, na kiasi cha masomo ya Injili ambayo amepokea tangu utotoni mwake; na pia uwezo wake wa kujifunza mafunzo ya Mungu. Miaka minne itaonekana ni mirefu, lakini Yosia alikuwa na umri wa 20 wakati alianza kazi yake. Hatusemi ya kwamba Mkristo kijana aendelee kwa miaka bila kukiri Mwokozi au kupeana injili kwa mtu yeyote, fikira kama hiyo itupiliwe mbali. Lakini inatakikana tuwe na msimamo mwema kabla ya kuanza huduma yo yote.

Wakati Yosia alipoanza kazi yake, hakuruhusu chochote kisimame mbele yake. Maovu mengine ambayo alitupilia mbali yalianzishwa na Sulemani na yalikuwa yamedumu kwa karne nyingi. Yosia hakuinamia utamaduni wowote wa watu na pia hakutaka kuwapendeza watu wake. Alihusika tu na matakwa ya Mungu na kumtumikia yeye. Alikuwa mwerevu na alifanya kazi yake kwa msimamo. Alikuwa na bidii na alifanya kazi yake kikamilifu. Aliharibu sanamu na madhebehu yote na hata alichoma mifupa ya makasisi ambao waliongoza ibada hizo za sanamu. (Habari za kazi zake zote zimeelezwa katika 2 Wafalme 23.) Hebu tufuate mfano wake katika kazi ya Mungu ambayo ametupa au atatupa kufanya. Hebu tufanye kwa maakini na ukamilifu kila ambacho Mungu ametupatia tufanye na tumtegemee yeye tu.

Ilimchukua Yosia miaka sita kusafisha nchi, lakini

hakustaafu kutoka kazi ya Mungu baada ya kumaliza kazi hiyo. Kazi yake iliyofuata ni utekelezaji wa hekalu na ibada ambazo zilifanywa ndani yake. Kulingana na mda wa maisha yake tunaona Yosia na tabia zake kuhusu Neno la Mungu wakati alipofahamu mafunzo hayo. Yosia alichukua neno la Mungu moyoni, alilijaribu kwake kwanza. Angelinganisha tabia zake na watu waliokuwa jirani zake na akajifurahisha kwa fikira kuwa alikuwa ni bora zaidi kuliko wao. Lakini badala yake alijinyenyekeza mbele za Mungu na kutubu. Wakati tumejiona tukiwa katika mwangaza wa Neno la Mungu na kulinganisha nafsi zetu na Bwana, hakuna nafasi ya kujishukuru. Baada ya Yosia kusikia Neno la Mungu, kusoma na kuelewa, alihakikisha ya kwamba kila mtu amesikia. Yeyote ambaye amejihakikisha katika ahadi na maonyo katika Neno la Mungu atahitaji kuwashirikisha wengine. Ni jambo muhimu sana na tunapaswa kuliweka katika nafsi zetu. Na mwisho, Yosia aliendesha ibada za hekalu kulingana na Neno la Mungu. Alisherehekea Pasaka kama vile Mungu aliamuru. Hatuwezi kumuabudu Mungu kama tunavyotaka. Lazima tumwendee na kumtii. Hakuna mahali katika Biblia pa uchaguzi wa kipekee au kibinafsi au "kufanya mapenzi ya mtu binafsi" katika tabia ya kuabudu. Kujaribu kumwambia Mungu ya kwamba tunajua kile anataka kuliko yeye mwenyewe, hayo ni makufuru makuu.

Sasa tuangalie kifo cha Yosia. Hili ni funzo la kwanza kutokana na Yosia ambalo ni baya. Katika 2 Nyakati 35:20 tutaona ya kwamba Yosia alikuwa amemaliza kulitunza hekalu kabla ya kufa. Alikuwa ni mtu wa nguvu za kutenda na alikuwa anatazamia mipango mipya. Hakumtegemea Mungu kumwongoza. La! lakini alifanya mapigano ya kijeshi na kutotii mapenzi ya Mungu. Matokeo yalikuwani kifo chake na kuanza kuanguka kwa ufalme wa Yuda. Ni

vizuri tuwe na nguvu za utekelezaji, lakini tutende mapenzi ya Mungu, bali siyo yetu. Ikiwa tunahitaji baraka kuliko laana, basi na tumtii Mungu.

Danieli na Marafiki Zake

Vijana wa Maombi

Danieli na wenzake (ambao wanajulikana kama Shadraka, Meshaki na Abednego) labda walipelekwa Babeli wakati walipokuwa chini ya miaka ishirini. (Waliitwa "watoto" lakini walikuwa watu wazima na waliweza kujua Neno la Mungu na sheria za Mungu na kuamua kumtii. Angalia Danieli 1.) Danieli aliishi miaka mingi huko Babeli, miaka ambayo alifanya utumishi kwa Mungu na mwanadamu. Jambo ambalo lilijulikana sana katika maisha ya Danieli, ni kutupwa kwake katika tundu la simba, kwa sababu ya ujasiri wa kuendelea kuomba Mungu wa pekee. Jambo hilo lilitendeka wakati alikuwa mzee. Ningependa kuonyesha katika somo hili ya kwamba Danieli na wenzake walikuwa watu wa maombi hata katika ujana wao.

Katika Danieli 2 tunasoma ya kwamba mfalme aliota ndoto ambayo yeye hakuielewa. Hata washauri wake hawangeweza kumtafsiria Nebukadreza maana ya ndoto yake, kwa hivyo akaamuru washauri wote wauawe. Amri hiyo iliwahusu Danieli na wenzake, ingawaje mfalme alikuwa hajawauliza wamsaidie (Danieli 2:13-16). Ni hatua gani ya kwanza aliyochukua Danieli kwa kupata jibu la swali hili? Yeye na Shadraka, Meshaki na Abednego waliomba. Hawakuomba tu ili kupata maarifa juu ya ndoto ya mfalme, bali waliombea uhai wao. Ni hatua gani

ya kwanza Danieli alichukua baada ya kupokea tafsiri ya ndoto? Aliomba. Mungu aliwapa maarifa baada ya kuomba tena ndipo akaenda kumuelezea mfalme ambayo alikuwa amejifunza. Danieli alikuwa mtu wa kuomba katika maisha yake yote. Mungu alimzawadia: "Kama vile hawa vijana wanne, Mungu aliwapa akili na ujuzi juu ya mafunzo yote na marifaa. Na Danieli alielewa maono yote na ndoto zote" (Danieli 1:17).

Je, ungependa uwe na akili na ujuzi katika mafunzo yote na hekima? Unayo matatizo yoyote katika mafunzo shuleni au chuoni au kazini? Siri ya Danieli ya ushindi inaweza kuwa siri yako, aliomba na hata wewe unaweza kuomba. Mwandishi anafahamu kutokana na ujuzi wake ya kwamba Mungu anafahamu sio tu ndoto na maono, sanaa na sayansi za zamani za enzi za Misri na Babeli, bali hata fizikia, kemia, hesabu na uchumi. Maombi yanaweza kutuletea msaada wa kweli katika kazi na masomo. Muulize Mungu akuonyeshe nini unaweza kusoma na ni mahali gani unapaswa kutumia wakati mwingi zaidi. Ikiwa utashindwa katikati ya mtihani, chukua mda uombe, muulize Mungu akufungulie fikira zako na akusaidie kukumbuka majibu yafaayo. (Haipendekezwi mtu kutumia wakati wa kusoma akiomba. Kitabu cha Mithali kinatuambia wazi ya kwamba, Mungu hapeani chochote kwa wenye uvivu. Maombi na masomo lazima yatumike pamoja.)

Baada ya kumaliza masomo na kupata kazi, maombi yana usaidizi mkubwa katika kazi. Mungu hawezi tu kutusaidia kutupatanisha na wafanyi kazi wenzetu, bali anaweza kutupa usaidizi katika taabu na mahitaji yetu. Mungu ni Muumba wa dunia nzima na anaweza kutusaidia kukabiliana na maumbile haya tukimtegemea yeye na kujinyenyekeza.

Bikira Maria

Je, Ubikira ni Jambo la Maana?

Ulimwengu unasema, "Ikiwa watu wawili wanapendana, basi maonyesho yoyote ya kukubaliana yanafaa kati yao." Je, Mungu ameunga tabia kama hii? Labda kusoma juu ya Maria bikira kunaweza kutusaidia kuelewa mapenzi ya Mungu kuhusu uhusiano wa haki wa watu wawili ambao wanapendana au wanataka kuoana.

Kwa kusoma juu ya mila za kuoana kwa wakati ule, watu wengi hudhani ya kwamba Maria alikuwa bado msichana mdogo wakati Yesu alipozaliwa. Hakuwa tu msichana wa hali ya juu katika uadilifu, bali pia alikuwa na uhusiano maalum na Mungu. (Ingelikuwa bora kama wasichana wadogo wote Wakristo wa wakati huu wangeliimba ule wimbo wa Maria katika Luka 1:46-55 kutokana na ujuzi wao wa Mungu.)

Maria hangechaguliwa kama mama wa Mwokozi, kama angelichukuliwa na mawazo ya ulimwengu wa sasa, ambayo hata yamewaingia Wakristo wengi wa siku hizi, kwamba watu wawili wakiwa wapenzi au wanataka kuoana, basi lolote kuhusu maonyesho yao ya kimwili linaweza kukubalika kwa mapenzi yao. Mungu alimheshimu Maria na usafi wake na anaweza kutukuza wavulana wo wote na wasichana ambao wanapenda kumfurahisha Mungu kwa kubaki bikira kabla ya kuolewa, kwa kuwasaidia wawe na ndoa ya haki na furaha.

Ndoa ya haki na furaha inaweza tu kupokelewa pakiwepo na umoja wa kiroho na pia umoja wa mapatano ya kimwili. Roho yetu ni ile sehemu yetu ambayo inaweza kukubaliana na Mungu. Na pia inachukua fikira na akili yetu ya kujua zuri na baya. Muungano wa karibu na umoja

wa kiroho hutokea wakati roho za wote wawili zimekuja karibu sana na Mungu na pia hivyo kuwa zimekaribiana sana. Kwa kipimo roho za wote wawili zinatii Neno la Mungu na kuongozwa na Roho Mtakatifu, na katika kipimo hicho, patatokea mapatano na umoja kati yao.

Sasa wakati wa kuanza kujenga umoja huu wa kiroho ni kabla ya kuolewa na hata kabla ya kuposana. Uhusiano wa kimwili huwa na maana kwa sababu una lengo la umoja wa kiroho. Jamii ya Kikristo haitakikani ipange kuoana mpaka watengeneze msingi wa kuoana kwa kuendeleza uhusiano wa kiroho na wajue ya kwamba wanaweza kusaidiana kila mmoja kuwa karibu na Mungu jinsi wakati unaendelea.

Maingiliano ya kimwili katika urafiki, hufupisha hali ya maendeleo ya uhusiano wa haki wa kiroho kwa njia nyingi. Kwanza, kukaribiana kimwili hivyo ni kusisimua mtu kwa raha na wote wawili hupoteza haja ya kiroho. Pili, ukweli ni kwamba uhusiano wao ni wa siri sana kwa hao wawili tu, ambao watajaribu kuuficha kwa wengine, unaweza kuwafanya wakaribiane sana. Wanaweza kuchukulia uhusiano huu wa karibu kimakosa kuwa ndio umoja wa kiroho, lakini unafifia baada ya kuoana na ndoa yao kuonyesha uhusiano wa “kiheshima” ambapo hapatakuwa jambo la kuficha. Hapo hawatakuwa na siri, na sasa watajikuta hawana jambo la maana la kushirikiana. Tatu, kwa vile sasa hawamfurahishi Mungu, hawawezi wakamsongea karibu kwa vile wako mbali na ushirikiano wake. Nne, kujisikia wenye makosa ambako fikira zao zitaweza kuamsha, kutakuwa kukiharibu maendeleo ya uhusiano wao wa ndoa. Mungu atabariki ile jamii ambayo inapanga mipango ya kuposana kama wakati wa maendeleo ya kiroho na umoja wa kijamii na kujaribu kuepuka kukaribiana kimwili nje ya ndoa. Hawatakuwa tu na kukaribiana kiroho bali furaha ya kweli ya uhusiano wa

kimwili pia.

Ndoa ni mfano wa umoja kati ya Kristo na Kanisa. Hii "enzi ya kisasa ya Kanisa" kwa hakika ni wakati wa "kuposwa" kwa Kanisa. Sherehe za ndoa hazitafanyika mpaka baada ya ufufuo (Ufunuo 19:7). Mtume Paulo alisema kuhusu Kanisa la Korintho, kuwa, "Nimekusukuma wewe kwa mme mmoja, ili nikuwakilishe wewe kama bikira kwa Yesu" (2 Wakorintho 11:2). Ni uzuri gani na furaha gani kwa Mungu wakati jamii ya Kikristo wanafanya kabla na baada ya kuoana kuwa mfano wa umoja wa Kikristo na Kanisa lake.

Yesu Akiwa na Umri wa Miaka 12

Maendeleo ya Kiroho Yafaayo

Tunasita kumuongeza Bwana wetu Yesu Kristo ndani ya kitabu hiki kwa sababu yeye ni Mungu na pia mwanadamu na kwa hivyo yuko juu kuliko mwanadamu yeyote. Ingawaje, maisha yake huwa mfano kwetu (1 Petro 2:21) na labda mafunzo machache juu ya Yesu Kristo akiwa mdogo, yanaweza kuwa na manufaa kwa maisha yetu, kama vijana, au wazee.

Hata kabla ya miaka kumi na miwili, Yesu Kristo "aliamukiwa na nguvu za roho, akijawa na maarifa na hekima" (Luka 2:40). Mara nyingi maendeleo yetu ya kiroho au maendeleo ya kiroho ya watoto wetu huachwa kuwa nyuma ya maendeleo ya mwili, akili, na maendeleo ya kijamii. Mungu alitufanya tuwe na msingi wa kiroho, kwa kuwa kupitia rohoni ndipo tunamtambua Mungu. Mwokozi wetu Yesu alikuwa akiendelea kiroho kwa miaka hiyo.

Vijana wa miaka kumi na mbili kwa wakati huo katika Israel waliruhusiwa kuhudhuria sherehe za ibada, kwa hivyo Yesu alienda Yerusalemu kwa maandalio ya Pasaka. Wakati wazazi wake waliondoka kwenda Nazareti, Yesu akabaki ndani ya hekalu. Ukamilifu wake wa maendeleo ya kiroho uanaonekana akiwasiliana na waalimu wa sheria: "Wote ambao walimsikia walishangazwa jinsi alivyoelewa na kujibu" (Luka 2:47). Kwa hivyo tunajua ya kwamba yeye alikuwa Mungu na hata alikuwa na hekima ambayo hatuwezi tukawa nayo. Kwa hivyo, je, hili silo funzo kwetu tuwe na akili katika kulisoma Neno la Mungu tukiwa vijana?

Labda sehamu ya mawaidha muhimu katika somo hili ni katika mistari ya 51 na 52: "Na akateremka nao, mpaka Nazareti, na akawa mnyenyekevu kwao, na Yesu akakua kimwili na kwa mawazo akiwa na upendeleo kwa Mungu na mwanadamu." Ikiwa Muumba wa dunia alikuwa mnyenyekevu kwa wazazi wake wa kiulimwengu, si hata sisi nasi tuwe watiifu kwa wazazi wetu? Mwanzo hawakuelewa, lakini yeye aliendelea kuwatii. Mwokozi Yesu aliendelea kukua (mstari 52) na hakumkosea mtu yeyote. Hebu nasi tufuate mfano wake ikiwezekana.

Wengine wanaweza kushangaa ni kwa nini Yesu alibaki nyuma bila kuwaelezea wazazi wake. Hapa ndipo hatuwezi kumfuata sana kwa vile yeye kama Mungu angeliweza kuwapa wazazi wake mawaidha ya kiroho, ambapo itakuwa ni makosa sisi kujaribu kufanya hivyo. Tunaweza kufahamu ya kwamba yale alifanya yalikuwa mapenzi ya Mungu kwa wakati ule. Labda Mungu alimuonyesha Yesu kufanya hivyo ili kuyafungua mawazo ya Yusufu na Maria. Kwa vitendo na majibu yao (katika mistari 48 na 50) tunaona ya kwamba walikuwa wamesahau, jambo muhimu kwa wakati huo, nafsi halisi ya mtoto wao. Walikuwa wamezoea

kumlea na kumtendea kama mtoto wa kawaida. Kwa kufaidika kwao wenyewe kiroho walihitaji kumwona jinsi alivyo. (Katika maisha yote ya Yesu, mpaka wakati huu, Shetani amekuwa na bidii sana akijaribu kushauri watu ya kwamba Yesu alikuwa mtu wa kawaida. Ni kwa kuamini alikuwa Mungu katika mwili wa mwanadamu, hapo ndipo tuna matumaini ya kuokolewa.) Yote ambayo Yesu alisema na kufanya yalikuwa ni mapenzi ya Mungu, na yalikuwa na lengo la utukufu wa Baba na ustawi wa akili na roho kwa mtu wa kawaida. Hili na liwe mwongozo wa matendo yetu yote.

Timotheo

Mfano kwa Wazee Wake

Kwanza kabisa tunampata Timotheo katika injili ya Matendo 16. Paulo alikuwa katika mkondo wa pili, wa safari yake ya umishionari. Timotheo aliokoka wakati Paulo alipoenda kule Listra. Timotheo alisifiwa sana na Wakristo wa Listra na Ikonia naye Paulo akamtaka Timotheo aandamane naye katika safari.

Timotheo hakuweza tu kuandamana na Paulo, bali aliweza kutumwa mahali tofauti tofuati kama mwakilishi wa Paulo (1 Wakorintho 16:10; 1 Wathesalonike 3:18). Timotheo aliendalea kuwa mwakilishi wa Paulo baada ya Paulo kufungwa jela (Wafilipi 2:19-23). Katika kifungu hiki cha mwisho, tunajifunza kwa nini Paulo alimwamini Timotheo kama mwakilishi na mjumbe wake. “Sina mtu mwenye akili kama mimi atakayetunza hali yenu vizuri kwa kuwa wengine hutafuta yale ya kuwapendeza bila kupendeza Yesu Kristo.” Wengi wa wale waliohubiriwa na Paulo walikuwa wameacha upendo na bidii zao za kwanza

na kuanza kuishi maisha ya kawaida ulimwenguni.

Barua za Paulo kwa Timotheo zinawapa mawaidha mazuri kwa Wakristo vijana. “Mtu awaye yeyote asiudharau ujana wake bali uwe kielelezo kwao waaminio katika uzima na mwenendo na katika upendo na imani safi” (1 Timotheo 4:12). Hapangekuwapo na “shida ya ujana” ikiwa vijana (na wazee pia) wangefuata mafunzo ya mstari huo na ikiwa vijana wangeweza kuonyesha mfano wa utakatifu kwa waumini wote. Mistari miwili ya kwanza ya 1 Timotheo 5 yaonyesha mwelekeo ambao yafaa vijana waonyeshe kwa watu wengine. “Msiwakemee wazee bali waheshimuni kama baba zenu, vijana wadogo kama ndugu, kina mama wazee kama wazazi, wasichana wadogo kama dada kwa uzazi.”

“Lakini zikimbie tamaa za ujana” (2 Timotheo 2:22). Watu wengi hufikiria juu ya tamaa za ujana kama tamaa za kimwili, bali pia tamaa ya kuwa na mali na kujulikana sana duniani, pia imeungana na tamaa za ujana. Katika 1 Timotheo 6:11, Timotheo aambiwa hasa aepuke tamaa hizi.

Mifano imetolewa kwa njia ambazo vijana wanaweza kutumia nguvu zao—kama wanajeshi wa Yesu Kristo, kama mkimbiaji katika mbio za kwenda mbinguni, na kama mkulima mwenye bidii ambaye hupanda mbegu ya Neno la Mungu (2 Timotheo 2:3-6).

Timotheo aliweza kufungwa wakati mmoja maishani mwake (Waebrania 13:23), lakini hatujui ni nini kilimtokea baada ya kifo cha Paulo. Bila shaka, Timotheo aliendelea kuwatunza watu wa Mungu na kufanya kazi ya “uinjilisti” maishani mwake hapa ulimwenguni. Na tuige mfano wa Timotheo na pia tutii mawaidha aliyopewa na Paulo.